# UHAKIKI WA MTINDO NA MAUDHUI KATIKA BAADHI YA TAMTHILIA ZA PENINA MLAMA

*Miriam B. Mwita*

## 1.0 UTANGULIZI

Katika makala hii tunachunguza fani na maudhui katika baadhi ya tamthilia za Penina Mlama.Tamthilia hizi ni: *Hatia (1972), Tambueni Haki Zetu (1973), Heshima Yangu (1974), na Pambo (1975).* Ingawa uhakiki wetu utazingatia hizo kazi ambazo tumezitaja hapo juu, tunafahamu fika kuwa, mtunzi huyu ameandika tamthilia nyingine nyingi na kuwa bado anazidi kuandika.

Penina Mlama ni mwandishi maarufu sana wa tamthilia nchini Tanzania. Aidha, yeye ni miongoni mwa wanawake wachache katika taifa la Tanzania waliopata kujitokeza katika uandishi wa kazi za kifasihi. Alianza kuonesha kipawa chake cha uandishi wa tamthilia alipokuwa shuleni na baadaye akiwa katika Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam.

Ni azma yetu kuchanguza baadhi ya kazi zake kwa sababu yeye ni miongoni mwa watunzi maarufu wa tamthilia za Kiswahili ambao wanatumia kipawa chao cha usanii, kusarifu taswira angavu zinazodhihirisha matatizo ya jamii ya Wantanzania na Afrika Mashariki kwa jumla. Tamthilia zote nne ambazo tunazihakiki katika makala hii ni ithibati madhubuti inayoshadidia na kubainisha matatizo ya jamii. Matatizo haya hususan yanatokana na usasa, hivyo, Penina anadhihirisha athari kadhaa katika *Hatia.* Kusema kweli, jambo la athari za usasa haliwezi kupuuzwa kabisa kwa kuwa mataifa ya Kiafrika hayana budi kuendelea pasipo kumwacha nyuma mwananchi ye yote. Suala la elimu na aina ya elimu inayotolewa kwa vijana, ni suala nyeti na linahitaji kuzingatiwa kwa dhati na kwa haraka. Suala hili limezingatiwa kwa uketo katika tamthilia ya Pambo. Aidha, suala la hadhi, heshima, haki, usawa na kuaminiana, ni baadhi tu ya maadili ambayo mtunzi ameyazingatia katika Tambueni Haki Zetu na Heshima Yangu.

Katika tamthilia hizi kuna ushahidi timilifu unaotuwezesha kuitetea hoja kwamba Penina Mlama, ni mtunzi na mhakiki wa hali halisi katika

jamii.Uandishi wake unaonesha uelewa wa mambo anuwai yanayowaathiri wanajamii katika vipengele mbalimbali vya maisha. Pamoja na haya, Penina Mlama alipohojiwa wakati fulani kuhusu lugha anayopenda kutumia katika uandishi wake, alisema kuwa, anapenda kutumia lugha ya Kiswahili kwa sababu analenga hadhira ya watu wanaozungumza Kiswahili. Pili, alisema ya kwamba, kwa kutumia Kiswahili, anaweza kujieleza vizuri zaidi. Aidha, kuhusu msimamo wake juu ya dhamira anazozishughulikia, alisema ya kwamba, anapoandika, yeye huchunguza tatizo lo lote lile ambalo analiona kuwa linawasumbua Watanzania wakati huo. Kwa kutumia sanaa, anajaribu kuonyesha tatizo hilo na kisha, ikiwezekana, atoe suluhisho ( Adeola 1990:74 – 91).

Baada ya utangulizi huu, tungependa kusema kuwa, ingawa katika makala hii, tumehakiki kila tamthilia kwa kuiweka katika nafasi yake bila kuihusisha na nyingine, mgawo huo ni wa kidhahania tu. Kusema kweli, tamthilia zote nne zinaingiliana kifani na kimaudhui. Mtunzi ameweza kusarifu mambo yanayomtatiza mwanajamii katika maisha yake ya kila siku. Mambo haya yanamtatiza na kumwathiri kwa namna nyingi. Penina Mlama ameyajadili matatizo haya kisanaa, na aidha, ameweza kupendekeza namna ya kukabiliana na baadhi ya matatizo haya. Tutaanza na mtindo.

## 2.0 UHAKIKI

### *2.1 Uhakiki katika Hatia*

#### *2.1.1 Mtindo*

Katika tamthilia ya *Hatia*, kuna mambo mengi yanayofungamana na mtindo wa kazi za kifasihi. Itakumbukwa kuwa, kila msanii ana msimamo, kwa hiyo, Penina Mlama anaihakiki jamii kwa namna yake mwenyewe. Katika uhakiki huu, tunahakiki tamthilia ya *Hatia* kimtindo na kimaudhui. Tamthilia hii, iliandikwa mwaka 1972. Tamthilia ya *Hatia* inaweza kumfaa mtu wa kiwango chochote kwa kuwa inahusu maisha ya watu wengi katika jamii na hasa vijana. Mwandishi, amefaulu kufanya hivi kwa kutumia wahusika anuwai pamoja na kuigawa tamthilia yake katika maonyesho sita tofauti. Kila onyesho, aidha, limepewa mandhari yake maalum. Pia, kupitia kwa mpangilio huu,mwandishi ameonyesha maisha ya jadi ya Watanzania. Kwa hivyo, tamthilia hii ni kama nyenzo ya kuhifadhi mila na desturi za Watanzania. Inavyobainika ni kuwa baadhi ya mila zinaanza kutoweka.

Mwandishi amedhihirisha umahiri wake kifani kwa kutekeleza mambo yafuatayo. Kwanza, ameigawa tamthilia yake katika maonyesho sita. Pili, amejitahidi kueleza mipangilio anuwai ya jukwaa. Tatu, amewachora wahusika wake kwa umakini kwa kuwapa sifa na tabia ambazo zinaangaza hali halisi za maisha yao. Kwa kufanya hivyo, anatoa picha ambazo hadhira yake wanaweza kujitambulisha nazo. Nne, ameteua maneno ya wahusika wake kwa uangalifu

huku akizingatia lugha itakayovutia. Mambo yaliyotajwa hapo juu humtambulisha Penina Mlama kama mwandishi aliyefaulu katika kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira lengwa. Ili tuelewe zaidi jinsi anavyofanya kazi hii muhimu, tutaanza kuzingatia onyesho baada ya onyesho.

Onyesho la kwanza linaanza kwa wimbo ufuatao:

> Sikilizeni! Sikilizeni!
> Hapa si kijijini
> Ohooo ohooo ohooo
> Sikilizeni! Sikilizeni!
> Hapa ni mji mkubwa ... (Uk. 7).

Wimbo huu una nafasi kubwa sana katika tamthilia nzima ya *Hatia*. Ni kutokana na wimbo huu ambapo tunaelezwa mazingira mapya mintarafu ya Cheja ambaye ni msichana aliyetoka kijijini. Mara moja hadhira wanatanabahishwa kupitia wimbo huu, kuwa hapa ni mjini na wala sio kijijini. Ni wazi kuwa mambo ya mjini na yale ya kijijini ni tofauti kabisa. Wimbo huu unaashiria, tahadhari kwamba sehemu hizi mbili, yaani mjini na kijijini, mambo yake ni tofauti sana na mtu hawezi kuchukua mambo ya kijijini na kuyapandikiza mjini kama yalivyo.

Aidha, katika onyesho hili, tunamwona Cheja ambaye ametoka kijijini na kwenda mjini. Huko mjini bila kujua matokeo na athari zake, anadhamiria kuishi kama wanamji. Ni kama anayaendea maisha kwa pupa hususan starehe za mji bila kutafakari matokeo ya vitendo vyake. Hatimaye Cheja anakutana na Juma, kijana wa mjini mbaye baadaye anatokea kuwa mpenzi wake. Hatima ya uhusiano huu ni mimba. Cheja anapomtafuta Juma ili amweleza kuwa ana mimba, Juma anamwambia kuwa hilo suala la mamba halimhusu kabisa:

> CHEJA : (polepole) Juma yale mambo ya siku ile nina mimba
> JUMA : Una mimba? Yangu mimi? (*Ananyamaza kama hakusikia kitu*)
> CHEJA : Sasa tupange la kufanya. Juma usijifanye kama hujui.
> JUMA : Haya, panga basi, panga, unasema tupange na nani? Haa! una maana upange na mimi, tafadhali sana dada tusiingiliane, yanakuhusu wewe mwenyewe ... (Uk. 8)

Pia, katika onyesho hili, Juma anamwambia Cheja kuwa, aseme kuwa mimba amepachikwa na mwajiri wake. Zingatia ushauri wa Juma:

> JUMA : Aaa *( kwa uovu)* hiyo ndiyo shida yako? Waambie kuwa kosa hilo limetendwa na mwajiri wako.
> CHEJA: Kaa! (*huku ameshtuka).*

JUMA : Ingawaje ana mke na watoto ile hutokea kwa hiyo wataamini tu. (Uk.9)

Katika onyesho la pili, mwandishi anatupeleka hadi kijijini kwao Cheja. Tunamwona mamake Cheja na wanawake jirani wakitwanga mahindi huku wana mazungumzo yao. Hapa pia tunamwona Cheja akiwasili nyumbani kutoka "Dalisalama" baada ya kupata mimba. Mama yake anamkaribisha kwa furaha ingawa anaonekana mchovu.

`Baada ya muda mfupi baba yake, Bw. Chowe, anawasili kutoka posta akiwa na barua ya simu. Barua hii inaonyesha kuwa Cheja ametoroka nyumbani kwa Bwana Sembuli na hawajui mahali alikoenda. Baba yake anataka kujua kwa nini ametoroka. Cheja ananyamaza lakini anapotishwa anasema:

CHEJA : Sikuweza kuvumilia kukaa nyumbani kwao ( anatazama chini).Hapana sikuweza.

BW. CHOWE: *(kwa kusita hali akiwa bado anatazama chini)* Bwana Se---Bwana Sembuli alinikosea kwa nguvu na sasa mimi mja mzito.

Jambo hili linamhuzunisha sana mama Cheja huku baba yake akiwaka kwa hasira. Mwisho, mwanamke wa pili anamshauri Bwana Chowe ayapeleke mambo hayo kwenye baraza la wazee.

MWANAMKE II: Hapana baba, hapana usiyachukulie mambo kwa ghadhabu. Usijihangaishe kumfuata unaweza kumkosa. Na nani ajuae, kwenye jiji kubwa kama "Dalisalama", lolote linaweza likutokee. Baraza letu la wazee mbona lipo na wewe ukiwa mmoja wao. Yafanyeni mashtaka haya kimila tu. (Uk.15)

Onyesho la tatu linatendeka katika uwanja nje ya nyumba ya Bwana Chowe na wazee wamekusanyika akiwemo Bwana Chowe na mwanae Mkami. Baraza hili lilitakiwa kutoa shauri kuhusu maovu aliyoyatenda Bwana Sembuli, yaani kumtia mimba Cheja. Huku baraza likiamua malipo atakayoyalipa Sembuli kwa kosa lake, Sembuli anatokezea na kuwaambia kuwa hayaelewi madai yao. Anasema kuwa Cheja aliondoka bila kuaga. Anaambiwa kuwa Cheja amefika nyumbani salama lakini ana mimba. Isitoshe, Sembuli anajulishwa kuwa ni yeye aliyempachika Cheja mimba. Sembuli anakataa:

SEMBULI : *(Kwa mkazo)* mimi nasema mzigo huo sio wangu, Narudia tena si wangu. Kwanza nashangaa kusikia kuwa Cheja ana mimba, tena nashangaa zaidi amepata wapi hii hadithi ya kunisingizia jambo ambalo sikufanya. ( Uk. 21).

Katika onyesho hili pia, mila na desturi miongoni mwa wanajamii zinasisitizwa sana. Wazee wanataka sana kufuata mila na desturi zao:

MZEE CHIMAISI : Wewe sahau kwanza ng'ombe. Sisi hapa hatufuati ng'ombe lazima tufuate mila zetu. Kila mtu lazima apewe haki yake na aridhike na shauri la baraza la wazee. Sembuli ameshitakiwa na anakataa kosa lake basi iliyobaki ni kutafuta msema kweli. (Uk. 21 – 22)

Mwisho, wanaamua kula kiapo ingawa Sembuli anaupinga uamuzi huu. Hata hivyo, analazimika kuandamana na wazee kwenda kwa mwapishaji ili kuweza kujua hali ilivyo.

Katika onyesho la nne tunakutana na mandhari ya porini. Mwandishi anatuchorea maandishi ya kichakani. Anaeleza kuwa kuna upenu. Picha inayobainika ni ile ya mahali maalum, mahali pa kuogofya na wala sio mahali ambapo wanadamu wanatembea kila siku. Kisha, tunawaona vijana wawili ambao ni wasaidizi wa mwapishaji wakitayarisha kiapo.

Mzee Chimaisi anaeleza sababu ya kutaka kiapo, aidha mganga anaeleza kuwa kuna aina nyingi za viapo, lakini wao watapewa kiapo cha kuopoa mawe yenye moto (Uk. 25). Maelezo haya yanatolewa kwa ajili ya Sembuli ambaye inaaminika kuwa haelewi mambo yanavyoenda kwa kuwa amekaa mjini. Kulowea kwake mjini huenda kumemfanya asahau mambo ya viapo.

Katika ukurasa wa 27, Sembuli anasema kuwa hana imani na mambo ya kiapo. Aidha, kwa hasira anasema, kama wanaamini kuwa ni yeye mwenye mimba, basi kwa upande wake, Mkami ndiye aliyempa dada yake mimba. Ikiwa kweli kiapo kingekuwa kinaaminika, Mkami angeapishwa kuwa siye aliyempa dada yake mimba. Jambo hili linazusha mapigano makali baina ya jamaa ya Sembuli na ile ya Cheja.

Onyesho la tano, linaonyesha ya kwamba baada ya kuona mambo yaliyotokea, Cheja aliamua kujinyonga. Anataka kufanya hivyo kwa sababu watu ambao wameumia hawana hatia. Uamuzi wa Cheja unafikiwa pale anaposema :

CHEJA : Acha waje wanipige na mimi. Hata kama wakiniua sijali kwa vile sina faida kuendelea kuishi. Kaka, baba yangu wamepigwa na kuumizwa. Vilevile, Bwana Sembuli naye ameumizwa. Wote hawa kwa ajili yangu----

> Nitathubutuje kuwaeleza kuwa hata mmoja kati yao si mwenye hatia? Mwenyewe Juma Bakari katulia Dalisalama hana wasiwasi (uk. 30).

Cheja anachukua kamba na kutoka, naye mamake akifuata huku akilia na kukimbia kwenda kumtafuta. Anamkuta na kumshika. Baadaye, Cheja anawaambia kuwa Juma Bakari ndiye aliyempachika mimba.

Katika kukimbia kwa Cheja ati kwenda kujinyonga, mwandishi amefaulu kutumia mchezo ndani ya mchezo. Bila kufanya hivi, ingekuwa vigumu kupata nafasi ya kueleza moja kwa moja kuwa aliyempachika mimba si Sembuli bali ni Juma Bakari.

Onyesho la sita ni hitimisho la tamthilia *Hatia*. Mambo yanatokea nje ya nyumba ya Bwana Chowe. Shughuli za onyesho hili zinaendelea baada ya mapigano kupungua baina ya aila ya Cheja na ile ya Sembuli. Bwana Chowe hajiwezi ana majeraha, hali kadhalika Mkami naye hajiwezi. Mzee Chimaisi anaagiza aletwe mganga. Wakati wakingoja mganga, Sembuli naye analetwa na watu wa upande wake wakitaka auguzwe kwani ana majeraha mabaya sana.

Katika onyesho hili pia, Cheja anaonekana akitolewa kule porini alikokuwa amekimbilia kwenda kujinyonga. Analetwa na wazee. Ukweli unathibitika pale Cheja anapokiri kuwa Juma Bakari ndiye aliyempachika mimba. Hapo hapo anaomba msamaha. Pamoja na hayo, Cheja anatoa uamuzi kuwa atajiunga na wanakijiji wa Majogo na kuanza maisha mapya. Sembuli anajitolea kwenda kumtafuta Juma Bakari na kumfundisha thamani ya maisha.

Baada ya kuzingatia mpangilio wa tamthilia ya *Hatia*, sasa tuangalie wahusika. Katika tamthilia hii, kuna wahusika wengi. Hata hivyo, uhakiki wetu hautashughulikia wahusika wote. Tutashughulikia baadhi tu ya wahusika, yaani Cheja, Mzee Chimaisi, Mzee Chowe, Sembuli na Juma. Cheja ndiye mhusika mkuu. Cheja, ni msichana ambaye amekwenda mjini kufanya kazi. Huyu msichana anavyooneka, ni mhusika mwakilishi. Anawakilisha wasichana wengi wa siku hizi ambao baada ya kupapia maisha ya mjini hupatwa madhila kama vile na janga la mimba na baadaye hushindwa pa kwenda kwani wenzao, yaani wale wavulana (wapenzi wao) huwakataa. Cheja, amedhihirisha udhaifu na unyonge wa wasichana wengi wa aina hii, ambao hujikuta wakiwa na rundo la matatizo, hususan ya kupata nimba mapema. Wengine hata huwasingizia baba zao au waajiri wao. Cheja ni mwongo tena ni mkosefu wa utu na uadilifu. Kama angekuwa na utu angekumbuka wema wa Sembuli. Hii ni kweli kwa kuwa alikuwa amekaa kwa Sembuli miaka miwili bila huyo Sembuli kumkosea.

Ingawa Cheja ameonekana kuwa mnafiki, tunamwona akiwa na sifa moja nzuri. Yeye anapotambua kuwa mambo yamemharibikia anaamua kuomba

msamaha. Pia anatambua ya kwamba kujinyonga hakutamsaidia kwa namna yo yote ile. Zingatia maneno yake hapa chini:

> CHEJA: Ninasema mwacheni. Iliyobaki naomba mnisamehe. Mnisamehe wazee wangu, hasa mzee Sembuli ... ( Uk. 38)

Pili, Cheja anaahidi kubadili hali yake na kwenda kijijini Majogo kushirikiana na wengine huko ili kuanza maisha mapya.

**Mzee Chimaisi** ni mhusika mwingine ambaye, anaonekana kuwa na busara na hekima ambayo inamtofautisha na wahusika wengine. Maneno yake ya busara yanamvutia msomaji kiasi cha kudhani kuwa ndiye mhusika mkuu katika tamthilia ya *Hatia*. Pamoja na haya ilikwishakudhihirika kuwa, Cheja ndiye mhusika mkuu.

**Bwana Chowe** kwa upande mwingine, ni mtu dhaifu kitabia, na aidha mwenye hasira. Kutokana na hamaki aliyonayo anataka kwenda "Dalisalama" kupambana na Sembuli. Isitoshe, hizo hasira zake zinamtuma kwenda kuua. Aidha, wakati wa mashauri, Chowe anaonekana kuwa na hamaki sana na laiti isingekuwa ushupavu wa Mzee Chimaisi kungejiri vita kwa muda mrefu na hivyo kusababisha majeruhi wengi na hata mauaji baina ya aila ya Cheja na Sembuli.

**Sembuli** ni mhusika mwingine ambaye anatuchorea picha nzuri ya Chowe. Hata hivyo, Chowe anaposikia singizio la binti yake kuhusu Sembuli, yeye anamkasirikia rafiki yake ambaye kwanza amesema kuwa wanaaminiana sana. **Sembuli** ni mtu anayeishi mjini na anaelewa matatizo ya mji. Anadhihirika kuwa mtu mwaminifu, na mwenye kufuata msimamo wake. Hali kadhalika, yeye ni mtaratibu.

Katika tamthilia ya *Hatia*, **wanawake** wanapewa nafasi maalum. Wao, wanaonekana kufuata na kuamini mila na tamaduni kwa dhati. Pili, mashauri yao yanakuwa na matokeo chanya na hivyo yanakuwa msaada mkubwa kwa Chowe na kwa jamii nzima. Penina Mlama amewapa wanawake nafasi maalum na kudhihirisha kuwa, licha ya kudunishwa na kuchukuliwa kuwa na hadhi ya chini, wanastahili kupewa nafasi ya kudhihirisha nguvu na uwezo wao wa kushauri na kuongoza.

Mwisho, katika uhakiki huu, tutamzingatia mhusika **Juma** ambaye anawakilisha tabia za wavulana wengi ambao hulowea mjini. **Juma** ni mhuni, anayewadanganya wasichana na kuwaharibia maisha. **Juma** hana utu wala heshima. Kwake yeye, wasichana ni vyombo vya kutumia ili kupata starehe. Anapokwisha kukinai starehe hizo, yeye huwatema kama mate pasipo huruma. vijana wenye tabia kama hii bado wapo. Kutokana na kuwepo kwa janga la UKIMWI, hii ni tabia ambayo hatuna budi kuipiga vita.

### *2.1.2 Lugha*

Katika *Hatia*, mwandishi ametumia lugha sahili. Lugha ya *Hatia*, si kakamavu ingawa mwandishi amejaribu kumpa kila mhusika lugha yake. Lugha inayotumiwa wa **Sembuli** na **Cheja** ni Kiswahili sanifu. **Sembuli** anazungumza Kiswahili sanifu kwa sababu amesoma na Cheja kwa kuwa amehusiana na wasomi na wakazi wa mjini. Mvuvi ana lafudhi yake. Kadhalika jamii ya Cheja inatumia lafudhi ya mashambani.Kwa jumla tunaweza kusema kuwa mtunzi ameimudu lugha yake.

### *2.1.3 Maudhui*

Maudhui ni jumla ya mawazo yanayojitokeza katika kazi ya fasihi. Tamthilia ya *Hatia* ina maudhui yenye vipengele kadhaa. Sehemu inayofuata itaangazia maudhui hayo.

### *2.1.4 Matatizo ya Usasa*

Wazo kuu mojawapo linalojitokeza katika tamthilia ya ***Hatia***, ni lile la matatizo ya usasa pamoja na ukuaji wa miji katika jamii ya Watanzania na Afrika nzima. Kwa hiyo dhana ya usasa inaangaziwa huku hali nyingine zikitumiwa na mwandishi kuwa na ufarisi wa kuangazia zaidi matatizo ya usasa. Katika tamthilia hii, tunaziona dunia mbili zenye mazingira tofauti. Dunia ya kwanza ni ile ya jadi na mapokezi ya kikabila, mahali ambapo ujamaa wa asili unachukua sehemu kubwa. Wenyeji wa dunia hii, wameshikamana na kutangamana pamoja na kuaminiana. Aidha, kila mtu anamjua mwenzake. Katika dunia hii, malezi ya wasichana ni muhimu sana. Kumlea msichana hadi kufikia umri wa kuolewa bila dosari, ni jambo la fahari sana. Dhana ya dosari ni pana katika malezi ya watoto katika jamii za Kiafrika. Hata hivyo, aghalabu humaanisha kushiriki tendo la ngono kabla ya ndoa. Kwa namna nyingine, kutokuwa na dosari kwa mtoto wa kike ni ile hali ya kudumisha ubikira. Endapo anaolewa huku akiwa bado ni bikira, basi binti huleta fahari na furaha kwa wazazi wake, hususan mama. Hapo ndipo alipokuwa Cheja. Wazazi wake walikuwa na matarajio makubwa kwake. Matarajio ya kumwoza akiwa bado bikira, jambo ambalo lingewawezesha kupata mahari na fahari kubwa kijijini.

Dunia ya pili, ni ile ambayo Cheja alikumbana nayo katika mazingira ya mji. Mji ni tofauti kabisa na shamba. Mjini watu wanatofautiana; aidha, wamejaa ubinafsi kwa sababu mbalimbali. Kusema kweli, mazingira ya mjini ni yenye kushinikiza watu wathamini na kupenda pesa na anasa. Hakuna shughuli iwezekanayo mjini bila pesa. Tunamwona Mvuvi akisumbuka kutafuta pesa.

Sembuli ni mfanyakazi, na hivyo shughuli yake kuu ni kutafuta pesa. Thamani ya mtu wa mjini huhesabiwa kwa fedha alizo nazo. Thamani ya Cheja, aidha, ni kule kuwa msaidizi wa jamaa ya Sembuli. Lakini kijijini, Cheja huhesabika kuwa mtu mwenye thamani. Thamani yake inatambuliwa na jamii yake nzima. Ni tegemeo la wazazi wake. Lakini zaidi kwa kaka yake. Anategemewa kiuchumi na familia yake, mahari yatakayotolewa wakati wa ndoa yake, yatatumiwa na kaka yake kuolea na aidha wazazi wake watapata sehemu yao. Cheja ni kitega uchumi kwa familia yake. Katika tamthilia hii, mwandishi anabainisha kuwa mazingira ya mji hayaambatani na utaratibu wa jamii ya jadi ya Watanzania. Aidha, anabainisha jinsi ambavyo usasa umeyavuruga maisha ya watu kule jijini. Kutokana na usasa, mifumo anuwai ya maisha imebadilika. Kiuchumi ni lazima mtu awe na pesa. Uhitaji wa pesa ndio kisa cha kumpeleka Cheja mjini. Bila pesa mtu hujiona maskini. Mwandishi anashadidia jambo hili kwa kumtumia Mama Cheja ambaye anasema:

> BI CHOWE : Ee jamani shauri ya uzee. Hivyo na mwanangu Cheja munamwona amekuwa mama mzima bado mnategemea nina nguvu za kutwanga tu. Kwanza hii yote shauri ya umasikini tu ... ( Uk.10)

Umaskini ndio unaomfanya Cheja kwenda mjini. Kule mjini akumbana na dunia mbili tofauti kabisa. Dunia hizi mbili ndizo msingi wa hatia kwa sababu dunia hizi zimeingiliana sana kwa upande mmoja lakini kwa upande mwingine zinatofautiana sana.

Katika hali hii, mazingira haya ya pande mbili, yaani ya kijijini na mjini, yanatuchorea mvutano na ukinzano katika tamthilia hii. Kwa namna nyingine, kuzuka kwa miji kumezua athari anuwai kwa maisha ya wananchi. Kwa mfano, kuna kufa kwa mila na desturi. Aidha, wananchi hawathamani uadilifu na utu tena. Ukosefu wa mambo haya kule mjini ni jambo ambalo hukinzana na jinsi hali ilivyo vijijini. Kijijini ni mahali ambapo watu bado wameungana katika vikundi vya kiaila, kiukoo, na kikabila. Hii ndiyo maana tunamwona Mkami na Sembuli wakizusha ugomvi baina yao kutokana na tamko la Sembuli *[kwamba yeye Mkami amempa dada yake mimba]*. Usasa, pia unapinga imani katika madawa ya viapo. Kinyume na msimamo wa Sembuli ya kwamba kiapo hakifanyi kazi, wanakijiji wanaamini kuwa kiapo ni mbinu thabiti ya kuthibitisha mambo.

Mvutano huu ndio unasababisha tatizo la Cheja na Juma. Tamthilia inaonyesha utovu wa nidhamu na uadilifu katika wakazi wa mjini. Cheja ametoka kijijini akiwa mwadilifu, lakini afikapo mjini anatumbukia katika mtego wa maisha ya kimji ambayo anayaendea kwa pupa. Mjini mila hazifuatwi. Juma naye amekwenda kuzurura mjini. Utu wake wote na hali ya

uadilifu vimetoweka. Amebaki kuwa mnafiki na hivyo mimba anayoibeba Cheja haimhusu sikio wala ndewe. Zingatia maneno ya Juma anapoambiwa ya kwamba Cheja ana mimba:

> JUMA : Jiendee kwa wazazi wako ukajitunze kama unaogopa kuendelea kukaa kwa mwajiri wako.
> CHEJA: Imekuwa si kitu kwako litakalonipata baadaye kumbe yote yalikuwa ulaghai ( Uk. 9)

Mwandishi ametuonyesha kuwa kilio cha Cheja si chake peke yake bali ni kilio cha jamii nzima. Jamii inauliza je, tufanye nini katika hii jamii mpya? Hata yale mambo ayafanyayo Juma na maisha anayoishi, yanahitaji marekebisho ya dharura ama sivyo mustakabali wa Tanzania umo hatarini. Sembuli, anawakilisha wanajamii ambao wanaona kuwa kuna haja ya kuwasaidia vijana kama Juma, endapo kutakuwa na mwamana katika jamii. Zingatia anavyosema Sembuli:

> SEMBULI : Tukimwacha atarudi tena kuwapotosha wasichana wengine na kuondoa amani mahali pengine ( Uk. 40).

Katika tamthilia hii, kuna funzo kubwa sana kwa wazazi, hasa wenye vijana wa kike. Mwandishi ameonyesha kuwa ni vyema kwa wazazi kutofanya haraka kuamini kila jambo wanalolisema wana wao hasa kuhusu mambo ya mapenzi. Mwandishi amebainisha kuwa ukosefu wa mwamana katika mambo haya ni hatari, hususan pale ambapo kijana wa kike anafahamu kuwa ana mimba. Aghalabu, msichana anapoulizwa kumhusu yule aliyempa mimba anaweza kudanganya. Ni lazima wazazi wajue ya kwamba binti anaweza kumsingizia mtu yeyote ili aweze kuinusuru nafsi yake.

*2.1.5 Nafasi ya mwanamke katika Jamii*

Tamthilia hii pia inatuonyesha kuwa hadhi ya wasichana katika jamii imejikita katika uwezekano wa kuwatumia kupata mali. Hivyo, mabinti ni vitega uchumi miongoni mwa jamii nyingi za Kiafrika. Binti hathaminiwi kwa kuwa ni binadamu mwenye uwezo na nguvu. Katika jamii nyingi za Kiafrika, wanawake wanaishi kwa ajili ya watu wengine hususan wanaume katika aila zake. Kama si baba, basi kaka au ndugu wa kiume. Mkami, kwa mfano, ni mwakilishi bora wa imani kuwa mwanamke ni kitega uchumi kwa manufaa ya mwanaume.

Katika tamthilia hii Mkami anathibitisha imani inayowafanya wanawake wadunishwe katika jamii. Zingatia maneno ya Mkami:

MKAMI : Kwa haraka) Ng'ombe saba, mbuzi tisa, na kuku watatu

MZEE CHIMAISI : ( Huku akicheka ) Babu vipi? Unataka ujipatie ng'ombe wa kuolea hapo hapo?

MKAMI : Ndio, kwanza huyu dada yangu angeolewa vizuri angepata, angepata zaidi ya hizo ... ( Uk. 18).

Wanawake, katika tamthilia hii, wanapewa hadhi na nafasi ya juu lakini wakati huo huo kwa upande mwingine, wanadhalilishwa mno. Kwanza, kwa mfano katika onyesho la pili tunaona kuwa mashauri yao yanafuatwa. *Mwanamke II* anamshauri Chowe asifanye mambo haraka kwani itakuwa vizuri kwenda kwa baraza la wazee. Huko atatoa mashtaka na kasha atasikilizwa na kupata suluhisho. Hata hivyo, kwa maoni yetu, mwandishi angezamia jambo hili kwa uketo zaidi kwa sababu, endapo wanawake wangepewa nafasi kubwa na muda wa kutosha wa kutoa ushauri wao, huenda maafa ya kupigana na kuumizana hayangetokea baina ya familia ya Cheja na ile ya Sembuli. Msanii anadhihirisha hali halisi katika jamii. Wanawakc hawapewi uhuru na nafasi ya kujieleza ama fursa ya kutoa mchango wao katika miktadha anuwai katika jamii.

Kwa muhtasari, mwandishi amezingatia athari za usasa katika maisha ya Watanzania na Wafrika wote kwa jumla.Athari za usasa ni nyingi, lakini uguraji kutoka vijijini kwenda mijini ni hali inayozua changamoto kwa watu wa aina zote. Aidha mjini kuna matatizo ya wasichana kupata mimba za mapema na kisha wakashindwa kuwashirikisha wenzao wa kiume waliowapachika mimba hizo. Wasichana hawa wanaishia kuwasingizia watu wengine wasiokuwa na hatia. Matokeo yake ni maafa makubwa kama anavyobainisha mwandishi. Mwandishi anapendekeza kuwa na busara katika kushughulikia matatizo ya usasa katika jamii.

Katika Tamthilia ya *Pambo (1975)*, Penina Mlama anaendeleza dhana hii hii huku akizingatia athari za elimu ya kisasa. Mwandishi amezamia swala la aina ya elimu inayotolewa kwa vijana. Anauliza : Je! Inakuwa ya manufaa katika maisha yao?

Muundo na mtindo wa tamthilia hii ni tofauti na ule wa **Hatia (1972)**, lakini kwa kiasi kikubwa maudhui yanaendeleza suala lilelile. Katika Pambo, Penina Mlama amedhihirisha ufarisi na ubunaji wa kiwango cha juu zaidi.

## 2.2 Uhakiki katika Pambo

### *2.2.1 Mtindo*

Katika sehemu hii, tutahakiki mtindo katika **Pambo**. Inabainika wazi kuwa, dhana ya kichaa imetawala tamthilia nzima. Mwandishi anasema kuwa, kichaa hiki ambacho kinatawala tamthilia hii sio kichaa kile cha kutumia nguvu na kufanya madhara, bali ni kichaa cha mawazo: Jinsi ambavyo mtunzi ameweza

kuendeleza wazo hili tangu mwanzo hadi mwisho wa tamthilia, imekuwa ni nguzo ya kudhihirisha kwa hakika ya kwamba, Penina Mlama ni mwandishi aliyekomaa na mwenye ujuzi wa kuimudu kazi yake.

Katika tamthilia hii kuna matumizi ya mbinu ya mchezo ndani ya mchezo. Mbinu hii imesaidia sana katika kupambanua muundo wa tamthilia nzima ambao unaweza kudhihirisha wazi lengo na nia ya mwandishi. Aidha, kwa kutumia mbinu hii, mwandishi kasana kazi yake kwa ufundi mkuu, kiasi cha kutowatamautisha wasomaji wake. Kimtindo, mwandishi amewahusisha wasomaji au watazamaji katika kuwatafuta akina Pambo kule porini. Mbinu hii ya kuwahusisha na kuwawezesha wasomaji na watazamaji inasaidia sana katika kuipa uhai tamthilia yenyewe.

Katika tamthilia hii, kuna maonyesho matatu. Katika maonyesho yote matatu, mwandishi amedhihirisha mandhari tofauti. Onyesho la kwanza linafanyika katika nyumba ya Pambo. Pambo amekaa huku akitazama Cheti na Joho pamoja na vichapuzi vingine ambavyo huvaliwa wakati wa mahafali ya kuhitimu masomo ya shahada ( digrii). Hapa, tunashudia kijimchezo cha Pambo kuhusu masomo aliyofaulu. Tunamtazama Pambo akiutazama mchezo huu. Kwa njia hii, tunapata fursa ya kuutafakari mchezo ulio ndani ya mchezo mkuu, yaani tamthilia ya Pambo. Pia, katika onyesho hili, tunashuhudia Maua ambaye tunakutana naye kwa mara ya kwanza, akikaribia gari la abiria katika kituo cha kuegesha mabasi. Mara ya pili tunamshuhudia Maua akiwa nyumbani kwa Pambo akijaribu kumsemesha lakini yeye hamjibu kitu bali anazungumza na Cheti na Joho lake. Kwa namna hii, Maua anautazama mchezo wa Pambo ambaye anacheka huku akiimba.

Katika mkabala huu, mwandishi anafaulu kuwahusisha rafiki za Pambo katika mchezo huu. Rafiki za Pambo wameweza kushiriki kuucheza na hivyo, si ajabu nao pia wanacheka na kuimba. Ama kwa kweli, tunawaona rafiki zake wengine hususan Pesa na Raha, ambao hatimaye wanaunganika na Pambo. Hali kadhalika, anaingia Blaza kwa Pambo. Naye anashangaa kumwona Pampo anaimba na kucheka bila kujali uwepo wa wenzake. Anajaribu kusema na Pambo lakini hapati jibu. Mwishoni mwa onyesho hili, tunawaona Wema na Maua wakigombana na kutukanana.

Katika onyesho la pili, msanii anatupeleka porini ambako tunakutana na Pambo, Pesa, na Raha. Ni wazi kuwa wamechoka, wamedhoofika na kuchafuka sana. Pia tunawaona akina Baba Pambo, Baba Raha na Baba Pesa wanafika porini. Wazee hawa wamekuja kuwatafuta watoto wao, lakini wanashindwa kuwashika. Hivyo wanaamua kutafuta mganga ambaye atawasaidia kuwashika watoto wao na kuwarudisha nyumbani.

Onyesho la tatu ni hatima ya tamthilia. Hapa, mwandishi anatuchorea mandhari ya porini ambalo Pambo na wanzake wanazidi kutokomea.Wazazi

wanaamua kumleta mganga ili awasaidie kuwarudisha watoto wao. Hapa kuna kijimchezo cha Pesa na Raha (Uk. 36). Kijimchezo hiki, kinaashiria hali ya wakati mgumu ambao unapotokea hata pesa hukosa thamani. Aghalabu, watu wengi huamini kwamba pesa ina uwezo wa kuleta raha maishani. Lakini sasa, pesa na raha havitoshi, kwa kuwa wote wawili wamekimbilia porini. Kijimchezo hiki kinapoisha, tunashuhudia mchezo wa mganga na kikundi kile cha wazazi wa Pambo wakiwa pamoja na Sikitu anbaye ni ndugu ya Pambo. Kikundi cha mganga, kinawatega watu wa kikundi cha Pambo kwa maarifa ambayo pia ni ya kiwendawazimu.Tamthilia inaisha.

Katika kuendeleza mtindo, tutageukia wahusika. Mhusika mkuu katika tamthilia hii ni Pambo. Pambo ana sura mbili. Kwanza ni Pambo mtu na Pambo cheti cha digrii. Sura hizi zinadhihirika katika mchezo ndani ya mchezo, mahali ambapo Pambo ni cheti cha shahada kadiri lilivyo joho la sherehe alilovalia Pambo wakati alipotunukiwa cheti cha digrii katika mahafali kule Chuo Kikuu. Kwa hivyo, kuna Pambo mtu pamoja na Pambo hali. Kupitia kwa Pambo mtu, tunaona Pambo hali ambapo elimu inakuwa pambo. Ni pambo kwa sababu, hata baada ya kufuzu, Pambo mtu hapati madaraka, raha, furaha wala pesa. Ni katika muktadha huu, ambapo sura ya Pambo mtu inatuchorea hali kamili ya vijana wengi hasa wasomi katika vyuo vikuu vya kisasa. Vijana wengi huvunjika moyo pale wanapokosa kupata madaraka makubwa na pesa nyingi baada ya kutia bidii masomoni chuoni. Wanajitahidi kwa lengo la kuyadhibiti maisha yao ya baadaye. Hali inayosawiriwa na Pambo inaakisi maisha ya kisasa. Kila kijana msomi huwa na matumaini ya kuwa na maisha bora hapo baadaye. Ubora huu unapokosekana, vijana huiona elimu yao kama Pambo tu. *Pambo* mtu ndiyo mhusika mkuu. Hali hii inawakilisha na kuidhihirisha dhamira na ujumbe wa tamthilia nzima. *Pambo* amepata kichaa cha mawazo. Maneno yake yanatuonyesha sababu ya kupata kichaa hiki. Kupitia kwa *Pambo*, mwandishi anatuonyesha mikinzano na migogoro inayojitokeza baina ya wasomi na matarajio yao binafsi na yale ya jamii zao. Wanajamii na vijana wasomi, wamefundishwa kuheshimu elimu na kisomo cha juu. Wamehakikishiwa kwamba kisomo ndicho ufunguo wa milango ya madaraka makubwa. Lakini katika ulimwengu wa sasa kinyume chake kinatokea, wapo wasomi wengi ambao wamesoma sana, lakini hawana madaraka makubwa wala pesa. Katika muktadha huu, *Pambo* anayakosa madaraka baada ya kupata shahada, anaugua kichaa.

Mhusika **Maua** ni msichana wa miaka 18 – 20. **Maua** ni mhusika mwakilishi ambaye anawakilisha wasichana wa umri wake. Wasichana hawa ni wale ambao wanapenda starehe, kutumiwa na kuwatumia vijana wenzao hasa vijana wa kiume. Kwa mfamo, **Maua** anaona ya kwamba kumiliki gari ndiyo

starehe. **Maua** anatamani vitu vingi sana ilhali anajua hata kama akifanya juhudi ya kila aina hataweza kuvipata.

**Raha** na **Pesa**, ni wahusika ambao mwandishi anawatumia kijazanda. Wahusika hawa ni wavulana wa miaka 10 – 15.Tunawaona wakiwa na uhusiano wa pekee na *Pambo*. Wahusika hawa, wanawakilisha tatizo la *Pambo*. **Pambo** anapenda raha, lakini tatizo analokabiliana nalo ni kuwa hana pesa za kutosha kugharamia raha anayoitaka. Ingawa Pambo hana pesa, **Raha** na **Pesa** ndio marafiki wake daima. Kila mara anafikiri kuhusu namna ya kupata raha pamoja na pesa. Hivyo, **Raha** na **Pesa** nao pia ni vichaa kwa namna fulani Kwa upande mwingine, **Raha** na **Pesa** ni vitu vinavyozua kichaa zaidi kwa Pambo.

**Wema** ni msichana anayeelekea kutofautiana na **Maua.** Yeye yu kama rafiki wa kweli wa **Pambo.** Anamwonea huruma na aidha anakuwa na uchungu kwa sababu ya hali ya kusikitisha inayomkumba **Pambo.**

**Wazazi** wa kina **Pambo** wanawakilisha wazazi katika jamii ya kisasa. Ithibati ya dai hili imekita katika msemo, "uchungu wa mwana aujuaye ni mzazi." Hata hivyo, **Baba Pambo** anaonekana kuwa mwenye busara anaposema: Tuweni wavumilivu. Tusiseme maneno mengi kwa vile tumechoka na kwa vile tumekutana na matatizo ... (Uk.45)

Mhusika mwingine muhimu katika tamthilia hii ni **Mganga. Mganga** amejitokeza kama mtu aliyekomaa katika Elimu ya Saikolojia. Badala ya kupendekeza madawa ya kiganga, anatumia mbinu nyingine mpya kabisa. Anaonekana kuwa mganga aliyekomaa katika taaluma ya tiba ya vichaa. Anawapumbaza wagonjwa wake kwa wimbo wa kiwendawazimu na hatimaye anafanikiwa kuwarudisha nyumbani. Ni kama mwandishi anapendekeza mbinu za kutumia katika kushughulikia matatizo ya vijana hasa wasomi. Vijana wasomi wanafanya kosa la kushindwa kupatanisha hali halisi ya maisha na ile hali dhahania ya maisha, yaani ya chuoni.

Mwandishi ametumia Kiswahili sanifu. Hata hivyo, amechanganya lugha kwa malengo maalum. Kwa mfano, amechanganya Kiingereza na Kiswahili. Wakati mwingine, anatumia maneno kama auti-"out", kushaini "shine", hivyo anadhihirisha uelewa wa lugha ya vijana wasomi.

### *2.2.2 Maudhui*

#### *2.2.2.1 Kichaa*

Mwandishi amezingatia masuala mengi katika tamthilia ya *Pambo*, lakini dhamira kuu inayojitokeza zaidi ni kichaa. Hata hivyo, mwandishi anasema kuwa kichaa hiki sio cha kuharibika akili, bali ni kichaa cha mawazo. Mwandishi amerudia maneno haya zaidi ya mara nane katika tamthilia.

Pambo anatamani kuwa na gari, pesa, nyumba nzuri, cheo kikubwa kazini, starehe za kila aina lakini vitu hivi vyote havipati. Sababu ya kuhitaji vitu hivi ni

kuwa amesoma na akapata digrii. Uchu huu unatokana na ile dhana kuwa elimu huambatana na kazi kubwa, gari na starehe za kila namna. Lakini ukweli unaodhihirika ni kuwa kuna matatizo mengi ambayo huwakumba wasomi kama **Pambo.** Matatizo ambayo kwa kweli huwakatisha tamaa vijana na hatimaye wanapata kichaa. Kuna sababu kadha wa kadha ambazo zimesababisha ukosefu wa kazi zenye hadhi kubwa kwa Pambo. Mojawapo ya sababu za tatizo hili, ni ile hofu waliyonayo wakurugenzi wa mashirika mbalimbali ambao hawakupata fursa ya kusoma na kupata shahada. Aidha, tatizo jingine ni ukweli kwamba, wapo watu wengine ambao hupewa nyadhifa zenye madaraka na mishahara mikubwa kwa sababu ya jamaa zao wenye vyeo na pesa nyingi, lakini sio kwa kutegemea kisomo na ujuzi wao.

**Pambo** anapata kichaa kwa sababu ya kukosa kazi ambayo ingemwezesha kupata pesa na hadhi katika jamii. Mwandishi anatuonyesha kuwa anashindwa hata kukodi nyumba yake binafsi na hivyo anakwenda kuishi na rafiki yake. Aidha, benki inashindwa kumwekea pesa zake. Haishindwi kwa kuwa ni nyingi mno, bali kwa kuwa ni chache mno. Katika msingi huu, Pambo hawezi kusaidia jamaa zake. Haya ni baadhi ya mambo ambayo yakizingatiwa kwa uangavu na makini, yanabainisha ukweli kwamba yanatosha kumtia mtu kichaa. Katika tamthilia ya *Pambo,* mwandishi anabainisha matarajio ya wazazi kwa watoto wao wanapowapeleka shuleni. Baba Sikitu anasema:

> Huyu Sikitu mtoto wangu kweli, lakini hana akili. Wewe unajua taabu tulizopata kwa **Pambo** kumsomesha mpaka kufika chuo kikuu, mimi nasuka majamvi, mama yako anapika vitumbua. Leo unathubutu kusema tuwaacheni waende wanakotaka? Na wewe pia una kichaa ( Uk. 28).

Ikiwa wazazi wanatusomesha kwa shida za kila namna, ni wajibu wetu kuwasaidia na kuwatumikia, hususan baada ya kupata kazi inayolipa mshahara mkubwa. Hata hivyo, tatizo ni kwamba, hata baada ya kusomeshwa kwa dhiki kubwa, kazi pamoja na ujira unaopatikana hautoshi kumkimu mfanyakazi, licha ya jamaa wanaomtegemea.

*2.2.2.2 Ushirikina*

Maudhui mengine katika tamthilia hii yanahusu ushirikina. Wema anaamini kuwa Pambo amelogwa ( Uk. 19). Hata Mama Doto, pia Baba Pambo anasema anaamini ni shughuli ya wachawi. **Baba Pambo** anasema: "Unamsikia anavyosema, uchawi upo kulingana na imani ya mtu binafsi" Tamthilia hii inatuonyesha kwamba, dhana ya ushirikina ina nafasi katika maisha ya Watanzania na Waafrika wote kwa jumla.

2.2.2.3 Udugu

Yamo pia maudhui ya udugu. Jambo hili linadhihirishwa na maneno ya Sikitu, ambaye anasema, "kwanza huyu kaka yangu mwenyewe sina faida naye wala yeye hajui kama ana ndugu yake aitwaye Sikitu. Sasa vipi mimi nipate taabu kwa sababu yake ..."(Uk. 29.)

Udugu umepoteza thamani yake kabisa katika jamii ya kisasa, kiasi cha watu kutojua jina la mdogo wao. Hali hii huenda inatokana na malezi mabaya na mielekeo ya wazazi wanaowaona watoto wao waliosoma kuwa bora zaidi kuliko wale ambao hawajasoma. Jambo hili, huleta dharau na chuki kati ya ndugu wa nyumba moja.

2.2.2.4 Uganga

Mwandishi anaelekea kudokeza umuhimu wa uganga wa Kiakili au Sayansibongo. Katika jamii ya sasa yenye vichaa vingi vya mawazo,daktari wa akili hana budi kupewa fursa pamoja na kuwezeshwa kwa lengo la kuwasadia wenye vichaa kama **Pambo.**

2.2.2.5 Matumizi ya pesa

Maudhui mengine inayojitokeza yanahusu matumizi ya pesa. Wazo kuu ni kuwa, kuna haja ya kupanga namna ya kutumia pesa.. Aidha, mwandishi anaonelea kuwa inafaa tamaa ya vitu ilingane na mapato ya mtu. Mtu mwenye tama kuzidi uwezo wake ataishia kupata kichaa kama **Pambo.**

2.2.2.6 Umoja

Umoja umeshughulikiwa kama maudhui muhimu katika tamthilia ya *Pambo*. Umoja unaonekana miongoni mwa wazazi wa Pambo, Pesa, na Raha. Umoja ndio unaowawezesha kuwarudisha watoto wao kutoka maporini. Pamoja na haya, itakumbukwa kwamba umoja hauwezi kuwapo ikiwa hakuna viongozi bora wenye kuthamini watu na utu. Hapa ndipo tunaona ukweli na nguvu za methali isemayo, "Umoja ni Nguvu na Utengano ni Udhaifu".

2.2.2.7 Nafasi ya mwanamke

Nafasi ya mwanamke imeangaziwa na mwandishi. Wanawake wote katika tamthilia hii wamepewa nafasi duni ya kujipodoa na kujipendekeza kwa Pambo. Isitoshe wao wanatukanana pasipo kujali utu wao. Hawana akili ya kupima na kutambua mwanamume mwenye uwezo. Aidha hawaelekei kuwa wamesoma. Kwa namna hii, Penina Mlama, ameshindwa kumtumainisha mwanamke. Yeye ameshirikiana na jamii kumdunisha mwanamke pale anapokubaliana na jamii kuwa mwanamke humtegemea mwanamume. Maua ni jazanda ya kujipamba. Huu ni mkondo pendwa wa mawazo kuwahusu wanawake. Nafasi anayopewa

Wema katika tamthilia hii ni ndogo mno. Hivyo haiwezi kuinusuru hadhi ya mwanamke. Kwa namna ya pekee, Penina Mlama, ameidunisha hadhi ya mwanamke.

Jambo hili linashadidiwa, kwa mfano, anapotumia maneno kama vile "Dogi Seksheni." Anapofanya hivyo, anaafiki kuwa wanawake ni kama mbwa. Ingetarajiwa kuwa, yeye kama mwanamke, angeteua maneno ya kuieleza sifa mbaya ya ukahaba pasipo kuwadunisha na kuwamithilisha wanawake na mbwa. Hali kadhalika, amewaonyesha kama watu wahitaji mno maishani. Anabainisha ya kwamba, uhitaji huu ndio unaowafanya wapigane kwa ajili ya kuwawahi wanaume kama Pambo. Mbali na haya, mwandishi hatuonyeshi jukumu la Mama Pambo, Mama Pesa, na Mama Raha kama wazazi wenza wa baba za vijana hawa waliopatwa na kichaa. Kwa namna hii, swali kubwa linalobaki kujibiwa ni , mama gani anayeweza kutulia mara apatapo habari kuwa mtoto wake amepatwa na kichaa? Kutowashirikisha na kuwawezesha akina mama hawa, ni udhaifu kwa upande wa mwandishi ambaye ni mwanamke. Hata hivyo, pamoja na udhaifu huu, mwandishi amefaulu kuwasilisha ujumbe alioudhamiria. Baada ya uhakiki wa *Pambo*, sasa tutahakiki *Tambueni haki Zetu (1972).*

## 2.3 Uhakiki wa Tambueni Haki zenu

### *2.3.1 Utangulizi*

**Tambueni Haki Zetu (1972)** ni tamthilia nyingine ya Penina Mlama. Tamthilia hii ni fupi lakini ina wahusika wengi ambao wanaweza kugawika katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni lile la watetezi wa haki na kundi la pili ni la wapinga haki. Tamthilia hii, aidha, inazingatia masuala ya kijamii, hususan haki na usawa katika jamii. Katika msingi huu, tunaiona `*Tambueni Haki Zetu*' ikishughulikia matatizo ya Watanzania. Tutaanza uhakiki wetu kwa kuzingatia mtindo wa tamthilia hii.

### *2.3.2 Uhakiki*

#### *2.3.2.1 Mtindo*

Katika kuzingatia mtindo alioutumia mwandishi, tunaweza kusema kuwa ametumia mtindo wa kawaida ambao waandishi na watazamaji wengi wameuzoea. Kama kawaida, mwandishi ameigawa tamthilia hii katika maonyesho kadhaa. Katika maonyesho haya ameyasawiri mandhari ya aina mbili. Katika mandhari moja, amesawiri kuzimu wanakoishi watu wa kale walioondoka wa karne nyingi zilizopita. Katika aina ya pili, amesawiri dunia ya kawaida. Mundewe anapoaga dunia na kutaka kuungana na hao mizimu waliopata kuishi katika dunia ya hizo zama za kale, mizimu wanamkataa, na hapo ndipo kiini cha *Tambueni Haki Zetu* kilipojikita.

Tamthilia inaanza kwa madai ya Mundewa kutaka kuingia kuzimu ili ajiunge na babu zake waliokufa zamani. Onyesho la kwanza linaisha kwa mabishano kati ya Mundewa na Sekulu na Mizimu. Hawa wanakataa kuwa Mundewa hawezi kukubaliwa kwani amekiuka heshima ya mizimu kwa kuanzisha mashambulizi dhidi ya Wakusa na Waboma.

Mundewa anaahidi kuwa ataweza kuthibitisha ya kwamba mashambulizi hayo ni haki na aidha yanastahiki kutambuliwa na kila mtu wakiwemo Mizimu.

Onyesho la pili hadi la kumi, ni ushahidi wa Mundewa juu ya haki ya kuwapiga Wakusa na Waboma. Sehemu hii, tunaweza kuiona kama mchezo ndani ya mchezo. Mundewa anadhihirishia dai lake kwa kuonyesha ubaya wa Wakusa na haja ya kuanzisha chama cha *ZETU* kwa ajili ya kujihami. Anazingatia matatizo ya chama. Matatizo ni pamoja na: Kuchanwa kwa hati ya mkataba wa udhamini wa Waboma kuwalea Watone, kufungwa na kutoroka kwa Mundewa kutoka jela, kusameheka kwa wapinzani wa chama cha *ZETU*, mapigano baina ya Watone na maadai yao na kufaulu pamoja na kurudishiwa heshima yao.

Onyesho la mwisho ni uamuzi. Mizimu bado wameachiwa uwanja wafanye uamuzi wa kutambua madai ya Mundewa ya kupigania haki. Lakini hadi hapa, mizimu bado hawajaona haki hii. Mizimu wanamfukuza Mundewa baada ya madai kuwa hana adabu wala hawatii. Mwisho kabisa Mundewa, anasema wazi ya kwamba, yeye, hawabembelezi Mizimu bali anawalazimisha watambue kwamba kupigania haki si makosa. Tazama hali inavyokuwa:

| | |
|---|---|
| SEKULU : | Ondoka! Ondoka |
| MUNDEWA : | *(Anamkatisha na anapaza sauti)* kwa nini hamtaki kutambua haki zetu. Haki, haki tupu ... |

Maneno haya yanatamkwa karibu na mwisho wa tamthilia. Mwisho huu, unatuonyesha ushindi wa Mundewa ambaye ni mhusika anayewakilisha makundi yanayoteseka chini ya udhalimu wa Walowezi.

2.4.2.2 Maudhui

2.4.2.2.1 Ukombozi

Katika kuzingatia maudhui ya tamthilia hii, tunaweza kuafikiana na mwandishi ambaye alipohojiwa na Shirika la Utangazaji la Marekani, alisema kuwa, "mchezo huu una mfumo wa kisiasa." Kwa hivyo, dhamira katika tamthilia hii ni ukombozi na matatizo yake. Kwamba watu wanadai haki zao na usawa. Hata hivyo suala hili amelisawiri kijamii, kisiasa na kiuchumi. *Tambueni Haki Zetu*, ni kauli ambayo inatokana na usemi wa Mundewa baada ya kukataliwa na Mizimu. Yatupasa tuone kuwa hii ni kauli ya madai na wala si nasaha. Kwa

hiyo, ni muhimu kujua ni kwa nini jambo hili si ombi bali Mundewa anadai Mizimu watambue haki za watu wa kizazi cha sasa.

Tukizingatia (Uk. 2) Wakusa ni wageni tu waliokuja kutoka mbali, Watoge waliwakaribisha nchini wakae wote kama ndugu. Wakusa walikuwa na mifugo na mali nyingi. Waliwagawia nyama na maziwa pia waliwafundisha jinsi ya kufuga ng'ombe (Uk. 2).

Ingetazamiwa kuwa Wakusa wawe ni wema zaidi ya hivyo wanavyoelezewa. Lakini wema wa Wakusa ukageuka na kuwa uadui wakati Wakusa walipoanza njama za kuwatawala Watone kwa nguvu. Mbali na kuwagawia nyama na maziwa, Mondota alipofariki alimwacha mwanawe kwa Waboma ili wamlee hadi atakapokuwa mkubwa. Ikiwa haya ni kweli, hiki ndicho kinakuwa kitovu cha uovu ambao unabainishwa katika *Tambueni Haki Zetu*. Licha ya kuwapa mamlaka ya kuwalea Watone, Mondota alifanya mkataba bila kujua. Ndiyo maana Sekulu anasema, "umewadharau watu walioaminiwa na babu zako..." (Uk.2)

Mwandishi anatuonyesha kuwa Mundewa ana haki kutenda "kosa katika fahari", na kujibu kwa kujivuna 'Ndiyo! Ingawa Mizimu wanaheshimiwa sana, tunaonyeshwa kuwa Mundewa alilazimika kuwadharau ili kuhifadhi hadhi ya Watone waliokuwa wakidharauliwa na kuteswa na "watu watoka mbali". Katika msingi huu, tunaona matatizo na juhudi za kujikomboa kwa Watone kutoka katika makucha ya walowezi wa Kikusa na Kiboma, kwamba mizimu wa Kitone bado wako upande wa maadui.

Ingawa Watone wako tayari kupigania haki zao, hawawezi kufanya hivyo. Jumbe anaeleza sababu za kutokata shauri kupigana:

> JUMBE : Wengi wenu mtashangaa kwa nini hatukukata shauri tupigane vita na Wakusa. Kwa sababu sisi Watone ni wapenda amani. Pili, bila kujipendelea, lazima tukumbuke kuwa hawa Wakusa wanakaa kivita na si ajabu watushinde nguvu. Zaidi ya hayo, Waboma wako upande wao ... (Uk. 11).

Tunaweza kumwona Jumbe kama kiongozi mwoga, lakini kuna ukweli katika maneno yake ambayo yanachochea tafakuri ya mbinu madhubuti za ukombozi na wala haitakuwa kuvamia tu kwa mori kama askari wa MajiMaji kama anavyoonyesha Ebrahim Hussein katika *Kinjeketile* (1969). Jumbe anazidi kufafanua mawazo yake kuhusu jambo hili katika mjadala unaofuata:

> JUMBE: Basi ni lazima tuangalie sana kuwa hatua tunazochukua hazituingizi motoni sisi wenyewe. Tusije tukajigeuza watumwa kwenye nchi yetu wenyewe.

MTONE: Lakini hata sasa sisi ni kama watumwa tu kwa mateso tuyapatayo.

JUMBE: Ni kweli, lakini sikilizeni, kwanza wageni wametuingilia vibaya sana ndiyo maana tumeamua mpango unaofuata sasa. Mnisikilize kwa makini. Tutaunda chama ambacho kitaitwa ZETU yaani "kilicho cha nchi, kilicho chetu"

WOTE: Ndiyo tuwapige Wakusa (Uk. 12).

Katika kujadili mbinu za kuwakabili Walowezi tunashuhudia suala la kisiasa la uongozi. Watone badala ya kutawaliwa na mori wa kupigana tu, wameona ni bora waanzishe chama cha ZETU. Chama hiki kinawaunganisha Watone wote. Kisha kwa umoja, walijifunza mbinu za kujihami. Ushahidi kuwa Wakusa ni maadui za Watone unadhihirishwa na Fonga ambaye ni kichocheo cha uchungu na nia ya kuleta umoja miongoni mwa Watone.

Mwandishi pia ameonyesha kuwa, siku zote kuna wale wanaopinga mapinduzi. Nono ni mhusika anayedhihirisha na kusisitiza jambo hili ingawa kwa maoni yake, anaona ni muhimu kuunganisha watu hawa pamoja kwani wanaweza kuwa hatari kwa jamii.

MUNDEWA: Hapana, tunahitaji umoja katika hali tuliyonayo sasa. Tusikubali mmoja wetu aachwe nje kwa sababu mtu mmoja anaweza kutuhatarisha sisi wote (Uk. 28).

Jibu hili linamdhihirisha Mundewa kama kiongozi shupavu na mwenye busara. Hizi ni sifa muhimu sana hasa wakati wa mapambano.

Mwandishi amebainisha ya kwamba, ukombozi wa kweli hupatikana kutokana na mapambano ya wenyeji husika. Jambo la pili ni kwamba, endapo mapambano baina ya Wakusa na Watone yatapamba moto, sharti watu wawe na umoja. Maoni ya mwandishi yameshabihiana na yale ya Ebraihim Hussein katika tamthilia ya *Kinjeketile* (1969).

Hata hivyo tofauti hapa ni kwamba, Mundewa amefaulu katika uongozi kwa kutunza nidhamu ya wananchi kinyume na *Kinjeketile*. Umoja ameupata kutokana na chama cha kisiasa cha ZETU na wala siyo kwa imani na itikadi ya maji. Chama hiki kinawawezesha watu kutafakari, badala ya kutenda mambo kwa pupa.

*Tambueni Haki Zetu,* ni tamthilia ambayo inaweza kuchukuliwa kuwa kama pendekezo la hoja ya kuwataka wagandamizaji watambue kuwa Watone, kama wananchi wa taifa lolote, wanastahili kutambuliwa na kuheshimiwa. Kila binadamu anastahili haki na usawa. Wadhalimu wote na wakoloni wa kila aina, pamoja na wagandamizaji sharti watambue haki za wanadamu popote duniani.

## 2.4 Heshima Yangu

*2.4.1 Utangulizi*

Heshima Yangu (1974) ni tamthilia ambayo imeandikwa na Penina Mlama. Ingawa tamthilia hii ni fupi, mambo anayoyashughulikia mwandishi ni marefu mno, hasa tunapoyazingatia kwa mujibu wa hali halisi ya maisha. Tamthilia hii inashughulikia masuala ya kijamii ambayo ni nyeti miongoni mwa wanajamii. Hata hivyo, mara nyingi hali inayojadiliwa kisanaa na Penina mlama, hufichwa kwa sababu za kibinafsi, huku ukali na dharau vikitumiwa kama mbinu ya kuficha vitendo vinayofedhehesha. Katika kubainisha ujumbe alionao mwandishi huyu, tutaanza uhakiki wetu na kipengele cha mtindo.

2.4.2 Uhakiki

2.4.2.1 Mtindo

Mwandishi wa kazi hii ametumia mtindo wa kawaida uliozoeleka na waandishi wengi pamoja na watazamaji au wasomaji wa tamthilia. Tamthilia ya *Heshima Yangu* imegawika katika maonyesho matatu huku kila onyesho likiwa na mandhari yake tofauti.

Onyesho la kwanza linatokea nje ya nyumba ya Mzee Isa, ambaye ni Babake Rukia. Katika onyesho hili, tunamwona Rukia akipepeta mahindi. Pia katika onyesho hili tunaambiwa kuwa Rukia amepata mpenzi kwa jina la Salum. Hadija, msichana wa makamo ya Rukia, anamwuliza kuhusu mapenzi yake na Salum. Hapo hapo tunamwona Hamza kakake Rukia naye akianza kujadiliana na Rukia kuhusu mapenzi yake na Salum. Hapa pia, Mzee Isa anatokea na anaposikia kuwa Rukia anapanga uchumba na Salum anapinga vikali sana uchumba huu.

Onyesho la pili, lina mandhari ya Rukia akitoka kisimani amejitwika ndoo ya maji. Rukia anakwenda kwa mwendo usio wa kawaida na anaonekana mwenye mawazo mengi sana. Salum anatokea lakini wao hawamwoni kwa haraka.

Rukia anataka kumwambia Salum kuwa baba yake amepinga uhusiano wao lakini anashindwa namna ya kumwambia jambo hilo:

> RUKIA : Nimekwambia usiropoke, Salum. *(Anageuka na kumpa mgongo)* Nisikilize Salum. Baba yangu amesikia kwa bahati mbaya juu ya urafiki wetu. Lakini amenikasirikia sana na kuniambia maneno ya kuumiza moyo wangu. (Uk.12)

Wakati wakiwa katika hali hii ya kuzungumza, Mzee Isa anatokea lakini wao hawamwoni.

MZEE ISA : (Anamwangalia Rukia ambaye amejiinamia). Mtoto wangu mwenyewe! *(Anamwangalia Salum)* mtoto wangu mwenye ... (Uk.13)

SALUM : ( Kwa woga) Mzee, hayo ni makosa yangu, ni mimi niliyem...

MZEE ISA : (Kwa ukali) Kelele, mwanaharamu wee! Kwanza huna hata haya ya kufanya haya.Toto lisilo na baba! Unathubutuje kumsongelea mtoto wangu mimi? (Uk.13).

Onyesho la tatu linakuja baada ya mzee Isa kumtukana Salum ambaye anaondoka na kwenda nyumbani. Onyesho hili, linatokea nyumbani kwa mama Salum ambapo tunamwona amekaa juu ya jamvi akisuka mkeka. Pole pole Salum huku akionekana mchovu anamsalimia mama yake, lakini mamake anagundua kuwa ana shida fulani.

MAMA SALUM : Nzuri, lakini kwanza nieleze shida yako. Mama anakazana aambiwe shida. ( Uk. 15). Salum anasema:

SALUM : Usiingiwe na wasiwasi, mama. Hizi ni shida zangu mimi mwenyewe ... kwa muda wa siku nyingi kidogo nimefanya mapenzi na Rukia.

MAMA SALUM : Rukia gani huyo? Mtoto – ( Uk. 16).

Hapo anaingia Mzee Isa kuja kumwambia amkataze Salum kuwa yeye hawezi kumwoa Rukia, kwani Mama Salum anajua hao ni mtu na ndugu yake. Mama Salum anasema kuwa yeye hakuta kuficha jambo hili lakini Mzee Isa alikuwa akimtisha. Sasa ilikuwa ni juu yake, lakini Salum hawezi kuoa dada yake.

Hata hivyo, Mzee Isa hakuja kwa nia nyingine zaidi ya dhamira ya kuhifadhi heshima yake. Wala haonekani kuwasikitikia watoto wake wawili ambao bila kujua wamependana, ilhali wao ni mtu na dada yake.

MZEE ISA : La, hasha! Ila nimemkanya vikali asiendelee kufanya mapenzi na Rukia.

MAMA SALUM : Sababu gani umempa kuhusu kumkataza.

MZEE ISA : Heshima yangu

Salum anatoa sababu aliyopewa, ati kwa sababu hana baba, na kwa hivyo hatakuwa na mtu wa kumsimamia katika sherehe.

Salum anasema alimwambia mama yake kuwa, kama anampenda, amwambie mara moja baba yake ni nani. Alitaka mama yake afanye hivyo mbele ya Mzee Isa. Salum alisema kuwa hata kama alikufa atakwenda amwonyeshe Mzee Isa kaburi halafu atafute baba zake wadogo ilmradi apate mtu wa kumsimamia sherehe anazozitaka Mzee Isa. Haya mambo yote atayatekeleza kwa lengo la kumpata Rukia. Ni wakati huu ambapo anaingia Rukia kuja kumwita Baba yake ili amfahamishe kuwa kuna mgeni. Mzee Isa anapotaka kuondoka, Mama Salum anamwambia asubiri waseme ukweli. Hapo Rukia na Salum wanajua kuwa wote ni watoto wa Isa na hivyo hawawezi kuoana.

Katika maelezo ya jarada la tamthilia hii wasomaji wanafahamishwa kuwa kiini cha tamthilia ya *Heshima Yangu* ni mapenzi baina ya vijana wawili, Salum na Rukia, ambao bila kujua kuwa wao ni ndugu wanataka kuoana. Mzee Isa ndiye baba yao wote wawili. Hawafahamiani kama ndugu kwa sababu Mzee Isa alimzaa Salum nje ya ndoa, kisha akakataa kukiri kuwa Salum ni mtoto wake. Anapinga uchumba wa Salum na Rukia kwa kisingizio kuwa binti yake hawezi kuolewa na mtu asiye na wazazi wala jamaa. Hata hivyo hatimaye ukweli unadhirika kuwa Mzee Isa ndiye baba ya vijana hawa wawili.

#### 2.4.2.2 Maudhui

##### 2.4.2.2.1 Heshima

Tamthilia ya *Heshima Yangu* ina maudhui mengi. Kwanza, mwandishi ameipa tamthilia hii, anwani ya *Heshima Yangu*. Swali muhimu la kujiuliza ni: heshima ya nani anayoizungumzia? Ingawa katika tamthilia ni Mzee Isa anayeng'ang'ania kudumisha heshima yake, ni wazi kuwa mwandishi anataka kutuonyesha kuwa kila mtu anastahili heshima. Rukia, Salum, Mama Salum, Mzee Isa na watu wote katika jamii wanastahili kupewa heshima. Ndiyo maana tunaweza kuuliza ya kwamba, kati ya wahusika tuliowataja hapo juu, ni yupi ambaye asingetaka kupewa heshima?

Jambo la pili, ambalo linabainika kutokana na tamthilia hii ni kwamba, ikiwa tunataka heshima, sharti tuwaheshimu wenzetu katika kila kipengele cha maisha yao. Ikiwa kweli Mzee Isa alithamini heshima, asingetenda mambo aliyotenda na Mama Salum. Isitoshe baada ya kuzaliwa kwa Salum, Isa hakuona umuhimu wa kumtambua mwanawe. Zaidi ya hayo, Isa alikataa kuhusiana naye kwa namna yoyote ile! Hali kadhalika, badala ya kumpa mtoto wake mwenyewe heshima, anamtukana na kumfedhehesha! Katika picha hii, Penina Mlama ametuchorea hali halisi ya maisha miongoni mwa baadhi ya aila. Kuna

wanaume wengi sana ambao wamezaa watoto na wanawake nje ya ndoa, kisha wanajifanya kuwa hawajali. Hata pale wanapowafahamu hao watoto wao, wanaishia kuwafedhehesha kwa matusi na dharau kocho kocho. Hata hivyo, ukweli haufichiki, huja wakajulikana na heshima yao ikavuja hata zaidi.

2.4.2.2.2 Ukweli

Maudhui mengine katika tamthilia hii ni kwamba, ukweli haufichiki, daima utajulikana. Ndiyo maana hatimaye, mwandishi anatumia maneno yafuatayo:

> MAMA SALUM:
>
> Salum mwanangu ningekuwa sikupendi mimi usingeishi kufikia umri ulio nao lakini ni upendo huo huo utakaokuletea huzuni ya muda lakini ya haki kwa sababu itakuponya kutoka balaa na kukupa heshima ya haki. Huwezi kumwoa Rukia. Baba yako huyu hapa, Mzee Isa (Uk. 19)

Kutokana na maneno ya mama Salum, mwandishi ametuonyesha watu ambao wanataka heshima lakini wao hawajali heshima za wenzao. Mzee Isa ni mmoja wao:

> MAMA SALUM:
>
> *(Anacheka)*. Wasema juu ya heshima saa hizi. Heshima unaijua wewe. Mimi siijui hata siku moja. Miaka yote hii nimeishi kwenye aibu ya kuwa na mtoto asiye na baba. Heshima yangu uliivunja wewe zamani sana. Sasa sielewi kwa nini unataka mimi nikusaidie kusitiri heshima yako yaangalie wewe mwenyewe. (Uk.18)

## 2.5 Hitimisho

Kwa jumla, Penina Mlama amedhihirika kama mwandishi wa tamthilia ambaye, anafaulu katika kutoa ujumbe anaoudhamiria. Haonekani kuwa na itikadi fulani maalum anayoifuata wakati anapoandika bali, huandika juu ya jambo lo lote lile ambalo analiona kama tatizo kwa jamii, tatizo ambalo jamii bado haina budi kulizamia na kulitafutia suluhisho mwafaka. Zingatia kwa mfano, suluhisho analotoa katika tamthilia ya *Hatia*. Aidha amezingatia tatizo la elimu miongoni mwa Waafrika kwa jumla. Jambo hili amelifanya vizuri sana katika tamthilia ya *Pambo*. Aidha, Tamthilia ya *Tambueni Haki Zetu,* imekuwa nyenzo ya kuonyesha kuwa kila mwanajamii, maskini kwa tajiri, anastahili kupewa haki na usawa. La sivyo, atapanga namna ya kudai hadi apate haki na usawa katika jamii. Mbali na kufaulu kwa Penina Mlama katika kutoa ujumbe wake, inabainika dhahiri kwamba, mwandishi, licha ya kuwa mwanamke, hatoi nafasi mwafaka kwa wanawake katika kazi zake. Ingekuwa bora endapo, angewachora

wanawake kwa njia ambayo ingewadhihirisha wakifanya juhudi katika kugeuza hali zao za uonevu. Kwa mfano, Mama Salum, angejaribu kumwendea Mzee Isa tangu hapo mwanzo alipomzaa Salum na kudai haki na heshima za mwanawe pamoja na yake binafsi. Hata hivyo, hatuwezi kusahau kuwa, Penina Mlama ni mwanamke na mwanajamii. Huenda athari za mfumo wa jamii yake imempata kwa kiasi fulani. Pamoja na haya, ni wazi kuwa mwandishi amejitokeza kama mwandishi anayetumia lugha kisanii kuelezea tajriba za Watanzania katika mazingira na miktadha tofauti. Aidha, Penina Mlama, amedhihirisha uwezo wake wa kueleza matatizo ya jamii yake na ya Afrika nzima.

## Marejeo


Adeola, J (1990) *In Their Own Voices: African Women Writers Talk*, James Currey Ltd, London.

Hussein, E (1969) *Kinjeketile*, Oxford University Press, Dar es Salaam, Nairobi.

*MULIKA*, Na. 11 – 17, Machapisho ya TUKI, Dar es Salaam University.

Nicholas, L. (1981) *Conversations with African Writers in Voice of America*, Washington D.C, USA

Penina Muhando, ( 1972) *Hatia*, East Africa Publishing House, Dar es Salaam

Penina Muhando, ( 1973) *Tambueni Haki Zetu*, Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

Penina Muhando, ( 1974) *Heshima Yangu*, East African Publishing House, Dar es Salaam.

Penina Muhando, ( 1975) *Pambo*, Foundation Books Limited, Nairobi.

Sengo, T.S.Y & Kiango, S.D. ( 1975) *Ndimi Zetu 2 Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili*, OUP, Dar es Salaam

## *SEHEMU YA TATU*

## *RIPOTI ZA UTAFITI, MIJADALA, BARUA NA MAONI*

---

### *Mwito wa Mhariri*

Mpendwa msomaji, jarida letu la *Mulika* limeanzisha safu hii ya *Ripoti za Utafiti, Mijadala na Maoni* ili kuwawezesha wasomaji wetu, wakiwemo walimu, wanafunzi, wakuza lugha na utamaduni na watafiti kushiriki katika kuchangia mawazo na maoni kwenye masuala muhimu yanayohusu lugha na fasihi ya Kiswahili. Katika toleo hili tumechapisha makala ya mwalimu Abdulrahim H. Taib kuhusu "Maisha ya Shaaban Robert na Falsafa Yake katika Maandishi" na Maoni ya Wanafunzi Saba kuhusu "Shaaban Robert na Vita na Ukoloni." Wasomaji wenye taarifa zaidi kuhusu Hayati Shaaban Robert au mabingwa wengine wa lugha na fasihi ya Kiswahili (k.m. Muyaka wa Muhaji, Hemed Abdallah, Mathias Mnyampala, Amri Abedi, Akilimali Snow-White, Siti binti Saad na wengineo) wanaombwa waziandike vizuri na kuziwasilisha kwa Mhariri wa *Mulika* ili ziweze kuchapishwa katika matoleo yetu yajayo. Shime, tushirikiane kukijenga Kiswahili na taaluma yake.